# Usindikaji Rahisi wa

# Muhogo

***Njia ya kuongeza uhakika wa chakula na pato la kaya***




TARP II - SUA Project

## UTANGULIZI

Muhogo ni zao ambalo huharibika upesi sana baada ya kuvunwa. Kwa mfano, ikiwa muhogo hautaliwa ndani ya siku 3 baada ya kuvunwa waweza kuharibika kabisa na kutupwa. Hii ni hasara kwa mkulima. Ingawa kuiacha mihogo shambani bila kuivuna hutumiwa kama njia ya kuhifadhi muhogo, njia hii si nzuri sana kwani hupunguza ubora wa mihogo kutokana na kukomaa mno na kushambuliwa na wadudu. Aidha ardhi huwa haiwezi kutumika tena kwa kilimo kwa muda wote huo wa hifadhi.

Matatizo yaliyotajwa hapo juu yanaweza kutatuliwa kwa kuusindika muhogo. Usindikaji wa mihogo ulioboreshwa waweza kumpatia mkulima au msindikaji aina nyingi za vyakula zinazoongeza thamani ya muhogo. Pia bidhaa hizi za muhogo zaweza kuhifadhiwa kwa muda mrefu zaidi.

## AINA ZA MIHOGO NA MATUMIZI YAKE VIJIJINI

Kuna aina nyingi za mihogo hapa nchini lakini zote zaweza kuwekwa katika makundi makubwa mawili. Makundi haya ni mihogo mitamu na mihogo michungu. Mihogo michungu mara nyingi inahusiana na kuwemo kwa kiasi kikubwa cha tindikali aina ya hydrocyanic. Tindikali hii ina sumu ambayo inaweza kuhatarisha afya au hata maisha ya mlaji.

Kwa upande mwingine mihogo mitamu ina kiwango kidogo sana cha tindikali hii na ambacho hupotea mara mihogo ikipashwa

joto. Kiwango cha tindikali hii iliyomo ndani ya mihogo ndicho kinachomfanya mkulima aamue aina ya matumizi ya mihogo katika sehemu inakolimwa. Kwa mfano, mihogo michungu hutumika kutengeneza unga wa ugali baada ya kulowekwa na kukaushwa. Kwa upande wake, mihogo mitamu yaweza kugegedwa, kuchemshwa, kukaangwa au kuchomwa na pia yaweza kutengeneza unga wa ugali baada ya kumenywa, kukatwakatwa na kuanikwa.

Pamoja na matumizi hayo hapo juu, tatizo lipo bado katika njia za kusindika muhogo. Njia nyingi zitumikazo ni duni, huchukua muda mrefu na hutoa bidhaa za viwango duni.

## TEKNOLOJIA RAHISI ZA KUSINDIKA MIHOGO

Utafiti shirikishi uliofanywa na watafiti wa Chuo Kikuu cha Sokoine Cha Kilimo (SUA) na Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa kuwashirikisha wakulima na wadau wengine, umewezesha mihogo kusindikwa kirahisi na kwa ubora ili kupata:

- Chipsi za muhogo
- Vibabu/kababu
- Maandazi ya muhogo, na
- Ugali wa unga mchanganyiko

Baadhi ya mashine zilizofanyiwa utafiti na kuboreshwa ni zile za kutengeneza chipsi na kusaga muhogo mbichi. Kati ya hizi kuna zile za mkono na ambazo huendeshwa kwa nguvu ya injini.

## a) Chipsi za muhogo

Utengenezaji wa chipsi unahusisha hatua zifuatazo: Kwanza chagua mihogo mizuri, imenye, ioshe na kisha katakata kwa kutumia mashine ya mkono au ya injini. Kaanga katika mafuta yanayochemka hadi zipate rangi ya dhahabu. Acha zipoe na ziweke kwenye mifuko safi ya nailoni. Waweza kuchanganya na karanga kisha funga mifuko. Chipsi hizi zaweza kukaa kwa zaidi ya wiki moja bila kuharibika.



## b) Vibabu

Utengenezaji wa vibabu unahusisha hatua zifuatazo: Kwanza chagua mihogo mizuri na mibichi, imenye na kisha isage kwa kutumia mashine ya mkono au ya injini. Baada ya hapo ikamue kuondoa maji yote na kisha iunde kwa mkono katika mviringo au umbo la yai na tumbukiza katika mafuta yanayochemka. Kaanga hadi viive kwa kubadilika na kuwa na rangi ya dhahabu. Acha vipoe na viweke kwenye mifuko ya nailoni. Viungo kadhaa vyaweza kuwekwa kwenye vibabu kama vile, tangawizi, vitunguu swaumu, karanga, nazi na nyama.

Vibabu vyaweza kuhifadhiwa kwa muda wa siku 3-4 bila kuharibika.



**c) Maandazi ya muhogo**

Ili kupata maandazi ya muhogo, changanya unga wa muhogo na unga wa ngano katika uwiano sawa. Weka maji, hamira na sukari na kanda hadi vyote vimechanganyika vizuri. Katakata maandazi kwa ukubwa unaopendelea. Kaanga maandazi yako kwa moto mkali kiasi hadi yawe rangi ya kahawia.



**d) Ugali wa unga mchanganyiko**

Muhogo waweza kutumika kutengeneza unga mseto kwa kuchanganya na nafaka nyingine ziliwazo katika eneo husika. Ili

kupata unga mseto, changanya chips kavu za muhogo na nafaka kwa kiwango unachopendelea na kisha saga mashineni. Ladha ya ugali wa unga huu itategemea mchanganyiko ulioutengeneza.

## HITIMISHO

Muhogo ni zao mbadala kwa wakulima wa Tanzania. Faida za muhogo ni nyingi na hasa katika kuongeza uhakika wa chakula na pato la kaya. Uboreshwaji wa njia za kusindika muhogo ili kupata aina mbalimbali za vyakula umeongeza nafasi ya muhogo katika kilimo hapa Tanzania. Shime sote tuongeze juhudi katika kilimo cha muhogo - MUHOGO NI MALI.


*Kimetayarishwa na:*

Watafiti wa Mradi wa Usindikaji wa Muhogo:
*(Dr V. C. K. Silayo, Prof. H. S. Laswai, Dr J. J. Mpagalile, Dr W. R. Ballegu, Dr P. J. Makungu, Mrs K. Mtunda, Mr D. Chilosa na Dr I. Nyborg)*



*Kimechapishwa na Kusambazwa na:*

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya
kwa Wakulima Wadogowadogo, Tanzania
(TARP II - SUA Project)
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
SLP 3151
Morogoro, Tanzania

Simu: 255 023 2600970
Faksi: 255 023 2600970

Toleo Namba: TS2-63